



UNIVERSITY EXAMINATIONS

SECOND SEMESTER 2023/2024 ACADEMIC YEAR

**SECOND YEAR EXAMINATION FOR THE DEGREE OF
BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)**

KISW 222: MOFOLOJIA NA SINTAKSIA YA KISWAHILI

STREAM: R

TIME: 2 HRS

DAY: WEDNESDAY (2.30-4.30PM)

DATE: 17/4/24

THIS QUESTION PAPER CONSISTS OF THREE (3) PAGES

PLEASE DO NOT OPEN UNTIL THE INVIGILATOR SAYS SO.



MAAGIZO: Jibu maswali MATATU. Swali la KWANZA ni la lazima.

SWALI LA KWANZA (ALAMA 30)

a) Fafanua maana ya dhana ya mofolojia na sintaksia **(Alama 05)**

b) Kwa kutolea mifano mwafaka, jadili aina za mofu za Kiswahili. **(Alama 07)**

c) Eleza dhana zifuatazo za mofolojia : **(Alama 08)**

i. Alomofu.

ii. Mofimu.

iii. Neno.

iv. Mofu.

d) Tathmini umuhimu wa kozi ya Mofolojia na Sintaksia kwa mwalimu wa lugha huku ukitolea ithibati mwafaka. **(Alama 10)**

SWALI LA PILI (ALAMA 20)

Ukitoa mifano kutoka lugha yoyote, eleza aina za ugeuzaji maumbo zifuatazo;

i. Ugeuzajimaumbo dondoshi. **(Alama 4)**

ii. Ugeuzajimaumbo chopekaji. **(Alama 4)**

iii. Ugeuzajimaumbo swali. **(Alama 4)**

iv. Ugeuzajimaumbo ubwete. **(Alama 4)**

v. Ugeuzajimaumbo rejeshi. **(Alama 4)**

SWALI LA TATU (ALAMA 20)

a) Huku ukitoa mifano kutoka lugha yoyote, eleza mbinu **NNE** zozote za uundaji wa maneno katika mofolojia. **(Alama 08)**

b) Eleza mfumo lugha na utendaji kulingana na Ferdinand De Saussure **(Alama 12)**

SWALI LA NNE (ALAMA 20)

Ziandikie sentensi zifuatazo kanuni miundo virai uzichoree vielelezo matawi: **(Alama 20)**

- i. Yohana mjanja alicheka sana.
- ii. Kibet anaenda sokoni.
- iii. *The man went to the market.*
- iv. Juma Analia.
- v. *He stole the book.*

SWALI LA TANO (ALAMA 20)

- a) Huku ukitumia mifano fafanua mofolojia ya kitenzi cha Kiswahili. **(Alama 08)**
- b) Kwa kutoa mifano mwafaka kwa kila mojawapo, fafanua dhana zifuatazo katika muktadha wa Sintaksia ya Kiswahili: **(Alama 12)**

- i. Sentensi sahili.
- ii. Sentensi changamani.
- iii. Sentensi Rejeshi.

